# HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 29/10/2021 KATIKA OFISI YA MCHUMI WA MANISPAA.

WAJUMBE WALIOHUDHURIA

1. Martin C.Mtani-Afisa Maendeleo ya Jamii wa Manispaa-M/Kiti
2. Clement C.Sanawa- Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi - Katibu
3. Frank Sichalwe - Afisa Elilmu Msingi wa Manispaa-Mjumbe
4. Andambike Kyomo -Mchumi wa Manispaa-Mjumbe

Wasiohudhuria;
Philipo Beno-Afisa Mazingira-mjumbe-Kwa Taarifa
Zawadi Nguaro-Afisa Kilimo Umwagiliaji na Ushirika-Kwa taarifa

SEKRETARIATE

1. Salum A. Mtumbey-Afisa Ugavi.
2. Andrew A.Nzali-Afisa Ugavi

AGENDA;

1. Kufungua Kikao
2. Kuthibitisha Agenda
3. Kumtambulisha Mjumbe wa Bodi ya Zabuni Frank schalwe-Mseo
4. Kupitisha miradi ya ujenzi wa madarasa yenye thamani ya Tshs.660,000,000.00 kwa kutumia Force Account.
5. Kupitisha mradi wa ujenzi wa kituo cha Afya Lilambo Tshs.450,000,000.00 na Mradi wa ujenzi wa kituo cha Afya Subira fedha ya (Tozo) Tshs.250,000,000.00
6. Kupitisha mradi wa ujenzi wa Matundu ya choo Tshs.59,200,000.00 na TEA Shs.80,000,000.00
7. Kupitisha mradi wa ujenzi wa Bweni katika shule ya msingi subiraTshs.80,000,000.00
8. Kupitisha mradi wa ujenzi wa Madarasa shule ya msingi Ruhira,Juhudi na Makinginda Tshs.120,600,000.00
9. Kupitisha mradi wa ujenzi wa mfumo wa maji Tshs.35,617,139.58
10. Kupitisha Ujenzi wa miradi yote hakwa kutumia FORCE ACCOUNT
11. Mengineyo
12. Kufunga kikao

KUMB.NA.SO/MC/BZ/08/2020/2021-KUFUNGUA KIKAO

Kikao kilifunguliwa na Mwenyekiti saa 8.00 Mchana na kuwakaribisha wajumbe kushiriki kikamilifu kwenye kikao hicho.

KUMB.NA.SO/MC/BZ/09/2020/2021-KUTHIBITISHA AGENDA

Agenda Kumi na moja(11) ziliwasilishwa na kusomwa katika kikao hicho na kuthibishwa na Wajumbe wa Bodi ya Zabuni.

KUMB.NA.SO/MC/BZ/10/2020/2021-KUMTAMBULISHA MJUMBE WA BODI YA ZABUN

Katibu wa Bodi ya Zabuni ambaye ni Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi,aliwaeleza Wajumbe kuwa kutokana na uteuzi wa Mjumbe wa Bodi ya Zabuni uliofanywa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa kwa Mujibu wa Sheria baada ya Muda wa Bodi ya Zabuni ya awali muda wake kufikia kikomo (Miaka mitatu),Hivyo Mkurugenzi alimteua Mwalimu Frank Sichalwe Afisa Elimu Msingi kuwa mjumbe wa Bodi ya Zabuni badala ya Zakia Fandey ambaye kwa sasa amehamia katika Mkoa wa Morogoro.

Baada ya utambulisho huo,Wajumbe wa Bodi walipokea taarifa hiyo na kuhaidi kushirikiana nae katika utekelezaji wa Majukumu ya Bodi ya Zabuni yaliyopo mbele yetu.

KUMB.NA.SO/MC/BZ/11/2020/2021-KUPITISHA MIRADI YA UJENZI YENYE THAMANI YA TSHS.660,000,000.00 KWA AJILI YA UJENZI WA MADARASA.

Katibu wa kikao aliwaeleza wajumbe kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Songea imepokea fedha kiasi cha Tshs 660,000,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa miradi mbalimbali ambayo inapaswa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo,na kuijadili kwa kina na kuagiza kuwa miradi inayotarajiwa kutekelezwa iainishwe ili ifahamike kila mradi umetengewa kiasi gani.

Baada ya majadiliano hayo,Wajumbe wa Bodi walipitisha ujenzi wa miradi hiyo ya ujenzi ili iweze kutekelezwa kwa wakati na kwa kufuata taratibu za manunuzi.Zilipitishwa kwa mchanganuo ufuatao:

ELIMU SEKONDARI.

| S/N | JINA LA SEKTA/MRADI | ENEO LA UTEKELEZAJI | FEDHA ZILIZOTOLEWA |
|---|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa madarasa 2 sekondari ya Msamala | Msamala | 40,000,000.00 |
| 2. | Ujenzi wa madarasa 2 sekondari ya Subira | Subira | 40,000,000.00 |
| 3. | Ujenzi wa darasa 1 sekondari ya Bombambili | Bombambili | 20,000,000.00 |
| 4. | Ujenzi wa madarasa 2 sekondari ya Chandarua | Chandarua | 40,000,000.00 |
| 5. | Ujenzi wa ya darasa 1 sekondari ya Londoni | Lizaboni | 20,000,000.00 |
| 6. | Ujenzi wa madarasa 2 sekondari ya Lukala | Tanga | 40,000,000.00 |
| 7. | Ujenzi wa madarasa 2 sekondari ya Luwawasi | Mwengemshindo | 40,000,000.00 |
| 8. | Ujenzi wa madarasa 2 sekondari ya Mashujaa | Mjini | 40,000,000.00 |
| 9. | Ujenzi wa darasa 1 | Mateka | 20,000,000.00 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | sekondari ya Mateka | | |
| 10. | Ujenzi wa darasa 1 sekondari ya Mbulani | Majengo | 20,000,000.00 |
| 11. | Ujenzi wa darasa 1 sekondari ya Ruvuma | Ruvuma | 40,000,000.00 |
| 12. | Ujenzi wa madarasa 2 sekondari ya Mfaranyaki | Mfaranyaki | 40,000,000.00 |
| 13. | Ujenzi wa madarasa 2 sekondari ya Mletele | Mletele | 40,000,000.00 |
| 14. | Ujenzi wa madarasa 2 sekondari ya Lizaboni | Lizaboni | 40,000,000.00 |
| 15. | Ujenzi wa darasa 1 sekondari ya Matarawe | Matarawe | 20,000,000.00 |
| 16. | Ujenzi wa darasa 1 sekondari ya Matogoro | Matogoro | 20,000,000.00 |
| | | **JUMLA** | **520,000,000.00** |

ELIMU MSINGI

| S/N | JINA LA SEKTA/MRADI | **ENEO LA UTEKELEZAJI** | **FEDHA ZILIZOTOLEWA** |
|---|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa madarasa 3 shikizi ya Nonga nonga | Mletele | 60,000,000.00 |
| 2. | Ujenzi wa bweni subira | Subira | 80,000,000.00 |
| | | **JUMLA** | 140,000,000.00 |

KUMB.NA.SO/MC/BZ/12/2020/2021-KUPITISHA MRADI WA UJENZI WA KITUO CHA AFYA LILAMBO TSHS.450,000,000.00 NA KITUO CHA AFYA SUBIRA TSHS.450,000,000.00

Katibu wa kikao aliwaeleza wajumbe kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Songea imepokea fedha kiasi cha Tshs 450,000,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa Kituo cha Afya Lilambo na Tshs 250,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Subira ambayo inapaswa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022.
Wajumbe walipokea taarifa hiyo,na kuijadili kwa kina.
Baada ya majadiliano hayo,Wajumbe wa Bodi walipitisha ujenzi wa miradi hiyo ya ujenzi ili iweze kutekelezwa kwa wakati na kwa kufuata taratibu za manunuzi.

KUMB.NA.SO/MC/BZ/13/2020/2021-KUPITISHA MRADI WA UJENZI WA MATUNDU YA VYOO TSHS.59,200,000.00 NA MRADI WA TEA TSHS.80,000,000.00
Katibu wa kikao aliwaeleza wajumbe kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Songea imepokea fedha kiasi cha Tshs 59,200,000,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa Matundu ya vyoo katika shule za msingi mbalimbali na Tshs 80,000,000.00toka TEA pia kwa ajili ya vyoo ambavyo inapaswa kujengwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022.
Wajumbe walipokea taarifa hiyo,na kuijadili kwa kina, na kuagiza kuinisha majina ya shule ambazo zinatarajiwa kupata miradi hiyo na kiasi cha fedha ambacho kitapelekwa katika shule husika.
Baada ya majadiliano hayo,Wajumbe wa Bodi walipitisha ujenzi wa miradi hiyo ya ujenzi ili iweze kutekelezwa kwa wakati na kwa kufuata taratibu za manunuzi.

KUMB.NA.SO/MC/BZ/14/2020/2021-KUPITISHA MRADI WA UJENZI WA BWENI TSHS 80,000,000.00

Katibu wa kikao aliwaeleza wajumbe kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Songea imepokea fedha kiasi cha Tshs 80,000,000.00
kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa Bweni la wanafunzi katika shule ya msingi subira.
Wajumbe walipokea taarifa hiyo,na kuijadili kwa kina, na kuagiza kuinisha jina la shule ambayo inatarajiwa kupata mradi huo.
Baada ya majadiliano hayo,Wajumbe wa Bodi walipitisha ujenzi wa mradi huo ili iweze kutekelezwa kwa wakati na kwa kufuata taratibu za manunuzi.

KUMB.NA.SO/MC/BZ/15/2020/2021- KUPITISHA MRADI WA UJENZI WA MADARASA KATIKA SHULE ZA RUHIRA,JUHUDI NA MAKINGINDA TSHS 120,600,000.00

Katibu wa kikao aliwaeleza wajumbe kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Songea imepokea fedha kiasi cha Tshs 120,600,000.00
kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa Madarasa katika shule za msingi za Ruhira,Juhudi na Makinginda
Wajumbe walipokea taarifa hiyo,na kuijadili kwa kina, na kuagiza kuinisha kiasi cha fedha ambacho inatarajiwa kupata katika mradi huo.
Baada ya majadiliano hayo,Wajumbe wa Bodi walipitisha ujenzi wa mradi huo ili iweze kutekelezwa kwa wakati na kwa kufuata taratibu za manunuzi.

KUMB.NA.SO/MC/BZ/16/2020/2021 KUPITISHA MRADI WA UJENZI MFUMO WA MAJI TSHS.35,617,139.58

Katibu wa kikao aliwaeleza wajumbe kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Songea imepokea fedha kiasi cha Tshs 35,617,139.58
kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa Mradi wa mfumo wa Maji katika shule za msingi.
Wajumbe walipokea taarifa hiyo,na kuijadili kwa kina, na kuagiza kuinisha jina la shule na kiasi cha fedha ambacho inatarajiwa kupata katika mradi huo.
Baada ya majadiliano hayo,Wajumbe wa Bodi walipitisha ujenzi wa mradi huo ili iweze kutekelezwa kwa wakati na kwa kufuata taratibu za manunuzi.

KUMB.NA.SO/MC/BZ/17/2020/2021 KUPITISHA UJENZI WA MIRADI KWA KUTUMIA FORCE ACCOUNT

Katibu wa kikao aliwaeleza wajumbe kuwa kufuatia maelekezo ya Serikali ili tuweze kutekeleza miradi kwa gharama nafuu, tulishauriana matumizi ya Force account itumike na kutendewa kazi wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo.
Wajumbe wa Bodi walipitisha taarifa hiyo ili iweze kutekelezwa kwa wakati na kwa kufuata taratibu za manunuzi.Miradi hiyo ni:-

i. Miradi ya covid-19 Ujenzi wa madarasa tshs 580,000,000.00
ii. Mfumo wa maji tshs. 35,617,139.58
iii. Ujenzi wa madarasa katika shule za ruhira,juhudi na makinginda tshs 120,600,000.00
iv. Mradi wa ujenzi wa Bweni Shule ya msingi subira TSHS 80,000,000.00
v. Ujenzi wa kituo cha afya Lilambo 450,000,000.00
vi. Ujenzi wa kituo cha afya Subira 500,000,000.00

vi. Ujenzi wa kituo cha afya Subira 500,000,000.00

KUMB.NA.SO/MC/BZ/18/2020/2021 MENGINEYO:

Mjumbe mmoja aliwasilisha hoja ya kuwa katika vikao vya Bodi inapaswa waandishi wa vikao vya Halmashauri waalikwe ili wawe waandishi wa mihtsari ya vikao vyote vya Bodi ili kuweka kumbukumbu sahihi.

Wajumbe waliipokea hoja hiyo na kuagiza kuwa katibu wa kikao kuwajulisha wataalamu hao kuhudhuria vikao vyote vitakavyoitishwa na Bodi.

KUMB.NA.SO/MC/BZ/17/2020/2021 KUFUNGA KIKAO

Kikao kilifungwa rasmi mnamo saa 9.00 mchana.

UMETHIBITISHWA

Martin C . Mtani
MWENYEKITI

Clement M.Sanawa
KATIBU

TAREHE: ..................................

KIKAO CHA KAWAIDA CHA BODI YA ZABUNI CHA TAREHE 22/10/2021.

AGENDA:

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha Agenda
3. Kuitambulisha Bodi ya Zabuni
4. Majukumu ya Bodi ya Zabuni
5. Taarifa ya Matumizi Mfumo wa TANEPS
6. Kupitisha Manunuzi ya Machinjio Tanga mfumo wa umeme TShs 10,773,000/=
7. Mengineyo
8. ~~At~~ Kufunga kikao.

Mahudhurio

1. MTANI, MC — MCDO — M/KITI [signature]
2. Zawadi Nguaro XMAICO — MAICO - mjumbe [signature]
3. Andambike Kyomo MEC — Mjumbe
4. Clement M. Sanana Ag.MSO — Katibu [signature]

Sekretariet

1. Salum Mtumbey SO — [signature]
2. ANDREW A. NZALI SO — [signature]
3.

KIKAO CHA KAWAIDA YA BODI YA ZABUNI CHA TAREHE 29/10/2021

MAHUDHURIO:

1. MTANI, MC — MCDO — M/KITI [signature]
2. Clement M. SANANA — AG. MSO — Katibu [signature]
3. Frank Sichalwe — MEO — Mjumbe [signature]
4. ANDAMBIKE KYOMO — Mjumbe [signature]
5.

AGENDA:

1. Kufungua Kikao
2. Kuthibitisha Agenda
3. Kumtambulisha Mjumbe Bodi ya Zabuni
4. Kupitisha Miradi yenye thamani ya TShs 660,000,000/=
5. Kupitisha Mradi wa Lilambo TShs 450,000,000/=
   Subira TShs 250,000,000/=
6. Kupitisha Matundu ya ~~Choo~~ vyoo TShs 59,200,000/=
   TEA 8 TShs 80,000,000/=
7. Kupitisha fedha za Lweri TShs 80,000,000/=
8. Kupitisha Ujenzi wa Madarasa Rubira, Juhudi na
   Malingumbwa TShs 120,600,000/=
9. Kupitisha mapokezi ya fedha ya Mfumo wa Maji TShs
   35,617,139.58
10. Kupitisha Ujenzi wa Mradi kwa Kutumia FORCE ACCOUNT
11. Mengineyo
12. Kufunga Kikao